

TAHARIRI

Makala za juzuu hili namba 19 toleo la kwanza zinahusu mada mbalimbali kuhusu lugha na fasihi ya Kiswahili na lugha za Kiafrika. Makala ya France inachunguza fonolojia vipandesauti katika lugha ya Kinyambo (lahaja ya Kimigongo). Makala inaonesha si tu minyambuliko inavyotokea katika neno bali pia jinsi mifuatano ya minyambuliko hiyo inavyotawaliwa na kanuni za kifonolojia. Kwa upande wake makala ya Mashauri inajadili michakato ya kifonolojia inayojitokeza katika maneno ya lugha ya Kiswahili. Michakato ya kiusilimisho na ile ambayo siyo ya kiusilimisho imejadiliwa. Kanuni kwa kila mchakato inaandikwa ili kuonesha bayana mazingira ya utokeaji wa michakato hiyo. Nao Ndomba na Chipalo wanazungumzia hali ya kupanda kwa kiambishi tangulizi cha kirai katika muundo wa kirai kibainishi. Katika kuonesha hali hiyo kwenye miundo ya kisintaksia, utafiti huu ulichunguza lugha za Kibantu za Kigogo, Kiha, na Kinyiha zinazozungumzwa Tanzania.

Kwa upande wake Devet anachunguza uainishaji wa vivumishi vya Kiswahili katika makundi ya kimaana. Kwa kurejelea mkabala wa Dixon (2004), ambao ameuboresha, anahitimisha kwamba vivumishi vya Kiswahili havina mipaka bayana na hueleza maana anuwai kutegemeana na muktadha. Kibiki anachunguza athari za kiimbo kwenye maana za kialami pragmatiki 'mh' katika mazungumzo ya Kiswahili. Makala imejikita zaidi katika mtazamo wa kipragmatiki. Mwandishi anabaini kwamba kiimbo kina athari kubwa kwenye maana katika mazungumzo ya Kiswahili.

Makala ya Karakacha, Zaja, Timammy na Wamutiso inachunguza usawiri wa mwanamke katika methali za Kiswahili na Kiarabu. Waandishi wa makala wanabaini kwamba usawiri wa mwanamke katika methali za jamii hizi unafanana sana, hii ni kutokana na athari za Kiarabu katika utamaduni na lugha ya Kiswahili. Makala ya Lyamuya inachunguza jaala za mashujaa zinazojitokeza katika tendi za Nanga, tendi hizo ni Rukiza, Mugasha na Kachwenyanja. Jaala mbalimbali zimebainika kupitia mashujaa wa tendi hizo.

Naye Ali anachunguza falsafa ya utu katika *Utenzi wa Mtu ni Utu* (1979) wa Ahmad Nassir Juma Bhalo kwa kutumia mtindo wa Iktibasi. Makala inaonesha jinsi Bhalo alivyochota moja kwa moja vifungu mahususi kutoka Kurani Tukufu na Hadithi za Mtume (S.A.W) bila ya kusema kwamba amechota kutoka humo. Faustine anaelezea namna Kezilahabi alivyotetea Uafrika kupitia maisha yake na katika kazi zake za fasihi alizoandika. Mwandishi anaonesha namna mtunzi alivyofinyanga fani na maudhui ya kazi zake yenye kuakisi mazingira, mila na desturi za Waafrika. Naye Mchepange anachunguza usawiri wa kijinsia wa dhamira zinazopatikana katika misemo inayoandikwa katika vyombo vya usafiri nchini Tanzania. Misemo mbalimbali kutoka katika vyombo hivyo imerejelewa kuhusiana na suala hili. Makala ya Mlaga inalenga kutatua changamoto zinazojitokeza katika kuihakiki itikadi kama kipengele cha kimaudhui katika kazi za fasihi. Kulifikia lengo hili makala inaonesha mikakati ya kubainisha vigambe vya kiitikadi katika matini mbalimbali za kifasihi. Mitazamo na umuhimu wa itikadi pia vimezungumziwa.

Wahariri, Juni 2021